

MKATABA WA KUUZA/KUNUNUA ENEO LA ARDHI

MKATABA HUU umefungwa leo tarehe¹⁵..... mwezi wa¹⁰....., 2023

KATI YA

FULBERTI JOSEPH AXWESO

.....

NA

ENGOITOI LIMITED

.....

SAHIHI YA MUUZAJI

F. Sule

SAHIHI YA MNUNUZI

[Signature]

MKATABA WA KUUZA/KUNUNUA ENEO LA ARDHI

MKATABA HUU umefungwa leo tarehe 15 mwezi wa 10, 2023

KATI YA

FULBERTI JOSEPH AXWESO, mkazi wa Karatu, Arusha, ambaye katika mkataba huu atajulikana kama "Muuzaji" tafsiri ambayo pale inapobidi itawahusisha warithi wake kwa upande mmoja;

NA

ENGOITOI LIMITED, kampuni iliyosajiliwa kwa sheria za Tanzania yenye namba ya usajili 167781829, S.L.P 414, USA River Arusha, ambayo katika mkataba huu itajulikana kama "Mnunuzi" tafsiri ambayo pale inapobidi itawahusisha warithi wake kwa upande wa pili.

PALE AMBAPO;

- A. Muuzaji ni mmiliki halali wa shamba lenye ukubwa wa mita 35 kwa 140 lililopo katika Kijiji cha Chemchem, Kitongoji cha Mbulumbulu, Kata ya Rhotia, Wilaya ya Karatu, Mkoa wa Arusha.
- B. Kwamba, Muuzaji amekubali na kuridhia akiwa na akili zake timamu kumuuzia Mnunuzi shamba hilo kwa gharama iliyotajwa katika aya ya kwanza (1) hapo chini.

Maelezo kamili kuhusu mipaka ya sehemu hiyo ya shamba ni kama ifuatavyo:

- (a) Upande wa Mashariki:
- (b) Upande wa Magharibi:
- (c) Upande wa Kaskazini:
- (d) Upande wa Kusini:


SASA BASI PANDE HIZI ZIMEKUBALIANA kama ifuatavyo:

1. Muuzaji atauza na Mnunuzi atanunua shamba lililopo katika Kijiji cha Chemchem, Kitongoji cha Mbulumbulu, Kata ya Rhotia, Wilaya ya Karatu, Mkoa wa Arusha, kwa gharama ya Shilingi Milioni Kumi tu.


Malipo haya yatafanyika kwa awamu mbili tu kama ifuatavyo:

- i. Awamu ya kwanza kiasi cha Shilingi Milioni Tano tu, tarehe 15/10/2023;
na

SAHIHI YA MUUZAJI



SAHIHI YA MNUNUZI.....



ii. Awamu ya pili kiasi cha Shilingi Milioni Tano tu italipwa baada ya miezi miwili, tarehe

15/12/2023

2. Malipo tajwa kwenye aya ya kwanza hapo juu yatalipwa kwa Muuzaji kwa pesa taslimu.
3. Mnunuzi anathibitisha kwamba amekwishakagua shamba tajwa hapo juu na ameridhia na kukubali kwamba baada ya kufanya malipo kulingana na makubaliano atapokea rasmi umiliki wa shamba hilo.
4. Muuzaji atawajibika kuwataarifu majirani wote wanaopakana na shamba hilo aliloliuza juu ya mabadiliko ya umiliki pamoja na wahusika wengine wote kama ndugu, jamaa, serikali za mtaa nk.
5. Muuzaji anathibitisha kwamba shamba hilo ni mali yake na kwamba halina madai yoyote wala halikuwekwa rehani na mtu yeyote yule. Pia inathibitishwa na Muuzaji kwamba hakuna dai la aina yoyote juu ya shamba hilo kutoka kwa mtu yoyote.
6. Iwapo itathibitika kwamba shamba hilo sio mali ya Muuzaji, basi Muuzaji atawajibika kumrudishia Mnunuzi fedha zote pamoja na riba kwa mujibu wa makadirio ya kibenki yatakayokuwa yanatumika kwa wakati huo.
7. Mkataba huu utatafsiriwa kwa mujibu wa sheria za Tanzania. Mahakama za Tanzania zitakuwa na mamlaka juu ya mgogoro wowote utakaozuka kati ya pande hizi mbili juu ya chochote kuhusiana na mkataba huu.

SAHIHI YA MUUZAJI

Fsulu

SAHIHI YA MNUNUZI

[Signature]

KWA USHUHUDA HUU, pande zote husika zimekubaliana kuweka sahihi zao katika mkataba huu katika siku na mwaka ulioandikwa hapo juu.

IMETIWA SAHIHI, mbele yangu ELIZABETH MAJUMA

Na FULBERTI JOSEPH AXWESO

Ambaye ninamfahamu / ametambulishwa kwangu na

CHRISTOPHER NDOCI

ambaye namfahamu leo tarehe 15 mwezi wa 10, 2023.

FSULE

MUUZAJI (SAHIHI)

MBELE YANGU: -

Jina: ELIZABETH MAJUMA

Anuani: 5143 DAR ES SALAAM

Sahihi: [Signature]

Wadhifa: WAKILI NA KAMISHNA WA VIAPO




IMETIWA SAHIHI na Mnunuzi

ENGOITOI LIMITED

Leo tarehe 15 mwezi wa 10 2023.

ENGOITOI LIMITED



Muhuri

Imesainiwa na:

Sahihi: [Signature]

Jina: CHRISTOPHER NDOCI

Anuani: 414 USA RIVER ARUSHA

Cheo: Mkurugenzi wa Kampuni

Sahihi: [Signature]

Jina: SHADWE AKWAWA

Anuani: 414 USA RIVER ARUSHA

Cheo: Mkurugenzi wa Kampuni

MBELE YANGU: -

Jina: ELIZABETH MAJUMA

Anuani: 5143 DAR ES SALAAM

Sahihi: [Signature]

Wadhifa: WAKILI NA KAMISHNA WA VIAPO



SAHIHI YA MUUZAJI FSULE

SAHIHI YA MNUNUZI [Signature]

MASHAHIDI WA MUUZAJI
JINA:

- 1. JAKOBUS MUKUNA
- 2. _____

UMUJUMBU
NICE

DATE
June

MASHAHIDI WA MINUNUZI

JINA:

- 1. CHRISTOPHER KAMUKUZI
- 2. ATONJA SIGI BURA

UMUJUMBU
JINJA

DATE
June

SAHIHI YA MUUZAJI

FRULE

SAHIHI YA MINUNUZI

[Signature]